# RISALA YA MGENI RASMI KWENYE MAADHIMISHO YA SIKU YA UKIMWI DUNIANI YANAYOFANYIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA KATA YA KIZWITE KATIKA VIWANJA VYA SHULE YA MSINGI KIZWITE TAREHE 01 DESEMBA, 2017

*Mheshimiwa Mgeni Rasmi,*

*Mwenyekiti wa CCM Mkoa,*

*Katibu Tawala wa Mkoa,*

*Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,*

*Viongozi wa Madhehebu ya Dini,*

*Makatibu Tawala wa Wilaya,*

*Wakurugenzi wa Halmashauri na Manispaa,*

*Viongozi wa Vyama vya Siasa,*

*Viongozi wa asasi za kiraia,*

*Wageni waalikwa,*

*Mabibi na mabwana,*

*Asalaam Aleykum, Tumsifu Yesu Kristo, Bwana Yesu Asifiwe.*

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo mahali hapa siku hii ya leo. Leo ni siku ya kilele cha maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani. Siku ya UKIMWI Duniani huadhimishwa Kimataifa ifikapo tarehe Mosi Desemba kila mwaka. Lengo kuu la maadhimisho haya ni kutafakari hali halisi na mwelekeo wa udhibiti wa UKIMWI Kitaifa na Kimataifa.

**Mhe. Mgeni rasmi**

Tanzania ikiwa ni mwanachama wa umoja wa Mataifa inaungana na Mataifa mengine yote ulimwenguni katika kuadhimisha siku hii muhimu. Madhumuni ya maadhimisho haya ni kuzidi kuikumbusha jamii, ulimwenguni pote kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI pamoja na

kukabiliana na changamoto zote tulizokabiliana nazo katika kipindi cha mwaka mzima.

**Mhe Mgeni rasmi**

UKIMWI umekuwepo Nchini kwa kipindi cha miaka zaidi ya therathini na tano sasa( 35) ni wazi kuwa ugonjwa huu unafahamika na watu wengi ikiwa ni pamoja na jinsi unavyoambukizwa.

Mwishoni mwa mwaka 2012 makadirio ya watu waliokuwa wameambukizwa UKIMWI walikuwa zaidi ya 1.5 milioni sawa na asilimia 5.1 ya watu wenye umri wa miaka 15 - 49. Kwa Mkoa wa Rukwa kiwango cha maambukizi ni asilimia 6.2 kiwango hiki kipo juu ya maambukizi ya UKIMWI Kitaifa. Njia kuu inayochangia maambukizi haya ni ngono zembe na unyanyapaa unaoendelea katika jamii. Takwimu hizi zimetokana na utafiti wa ugonjwa wa UKIMWI na malaria uliofanyika Mwaka 2012, ambapo katika Mkoa wa Rukwa maambukizi yameongezeka kutoka asilimia 4.9 Mwaka 2008 hadi

kufikia 6.2 mwaka 2012. Hii ni hali ya kutisha katika jamii.

**Mhe. Mgeni rasmi**

Ugonjwa wa UKIMWI umeendelea kuwa tatizo kubwa katika jamii yetu na lina athari kubwa kijamii, kiuchumi na kimaendeleo kwa ujumla.

Ugonjwa huu katika Mkoa wetu umeendelea kumaliza nguvu kazi na kuziacha familia katika hali ya umasikini na kusababisha watoto wanaishi mazingira magumu na hatarishi hususani watoto wa mitaani.Sababu zinazosababisha maambukizi kuwa juu Mkoani kwetu ni kama zifuatazo:-

- Kufanya ngono zembe
- Umaskini
- Mwingiliano wa shughuli za kibiashara
- Kuwa na wapenzi wengi
- Unyanyapaa wa WAVIU na Jamii inayowazunguka

- Mila na desturi zilizopitwa na wakati (kama kurithi wajane na wagane)
- Ulevi uliopindukia

**Mhe. Mgeni rasmi**

Ujumbe wa mwaka huu unasema" **CHANGIA MFUKO WA UDHAMINI WA UKIMWI: OKOA MAISHA, TANZANIA BILA UKIMWI INAWEZEKANA" Dhima kuu ya** Kauli mbiu hii ni kuhamasisha jamii katika uchangiaji wa Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI Nchini (AIDS Trust Fund-ATF). Mfuko huu ulianzishwa kupitia marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kuthibiti UKIMWI Na. 6 ya mwaka 2015. Lengo la kuanzishwa kwa Mfuko huu ni mkakati wa serikali kuwa na Mfuko wake na sio kutegemea wafadhiri kwa asilimia mia moja.

**Mhe. Mgeni rasmi**

Maadhimisho haya hutoa fursa ya kutathmini hali halisi na mwelekeo wa udhibiti wa UKIMWI vilevile kubaini changamoto, mafanikio na mikakati mbalimbali katika kupambana na janga hili. Siku hii pia hutoa nafasi ya kuwajali yatima waliotokana na janga la UKIMWI.

**Mhe. Mgeni rasmi**

Jumla ya wananchi 308727 wamejitokeza kupima VVU ikiwa wanawake 167623 na wanaume 141104 kwa mwaka2016/2017. Waliokutwa na maambukizi ni 4620 Wanawake 2602 Wanaume 2018. Hali ya upimaji wa VVU kupitia huduma za tohara kwa wanaume. Waliopimwa ni 33784 na matokeo ya waliokutwa na maambukizi ni 32. Waliofanyiwa tohara ni wenye miaka 10-29 na 30+ jumla ni 35180 kwa mwaka 2016/2017. Hali ya watoto waliopata huduma hadi kufikia septemba 2017 jumla yao ni 1346 ikiwa Wakiume ni 638 na Wakike ni 708. Watoto walionzishiwa dawa hadi kufikia Septemba

2017 jumla ni 1330 ikiwa Wanaume ni 631 na Wakike ni 699.Hali hii inaonyesha kuwa jamii kwa sasa imekuwa na mwamko wa kujua hali za afya zao.

**Mhe. Mgeni rasmi**

Mkoa umekuwa ukifanya uhamasishaji wa mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kutumia gari la sinema Jumla ya vijiji 89 na Kata 36 zimefikiwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Elimu ya tohara kwa watoto walio chini ya miezi sita inatolewa kwa ajili yakuondoa kundi kubwa la wanaume wasio fanyiwa tohara ikiwa ni kinga ya maambukizi ya UKIMWI kwa asilimia 60. Mkoa pia umeendelea kutoa misaada ya kibinadamu kwa vikundi WAVIU vya 34 kwa gharama ya Shilingi 43,000,000 na watoto yatima wapatao 611 wamelipiwa ada za shule jumla ya Shilingi 24,070,000.

**Mhe. Mgeni rasmi**

Shirika la Kimataifa la UNAIDS, liliweka malengo kwa ajili ya Nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara, ifikapo 2020, Nchi hizo ikiwemo Tanzania ziweze kuwatambua kwa asilimia 90 ya watu wote wanaoishi na maambukizi ya VVU, kuhakikisha kwamba asilimia 90 ya watu wanapatiwa dawa za kupunguza makali ya VVU na wanazitumia kwa ufuasi unaotakiwa na kuhakikisha asilimia 90 ya watu hao wenye maambukizi ya VVU hawanyanyapaliwi.

**Mhe. Mgeni rasmi**

Katika kufikia malengo haya ya 90 tatu, Lengo la kwanza la upimaji wa VVUndiyo lenye changamoto nyingi ikiwemo kuwafikia watoto wote, vijana na makundi yote maalum. Mikakati ya kufikia 90 tatu imekuwa ikitekelezwa na Katibu Tawala wa Mkoa na kwa kupitia wadau wetu wakuu wa maendeleo Walterreed, Mkapa Foundation, Peace and Relief, Lichide, Shdepha, CEELS, JSI, na wangine wengi.

**Mhe. Mgeni rasmi**

Napenda kukushukuru kwa kukubali kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho haya Mungu akubariki sana pia napenda kutoa shukrani kwa wageni mbalimbali kwa kushiriki pamoja nasi bila kuvisahau vikundi vyote vilivyotoa burudani Mungu awabariki sana.

**TANZANIA BILA UKIMWI INAWEZEKANA, RUKWA BILA MAAMBUKIZI MAPYA YA UKIMWI INAWEZEKANA**, tushiriki kwa pamoja katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

Naomba kuwasilisha.